Enyi wachungaji msiogope

Siku kuu ya Noeli

Eugène AMPIRE Bisimwa



2



Kiitikio

Enyi wachungaji msiogope, kwani, tazameni
habari njema ya furaha ninayowapasha:
Haya, nendeni Betlehemu, huko kazaliwa Mwokozi
wa dunia, ndiye Kristu, Masiya na Bwana.

1

Nendeni huko, mtamkuta mtoto Yesu akifunikwa vitambaa
nakulazwa pangoni mwa wanyama.

2

Walipofika huko, walimkuta mtoto Yesu akizungukwa na
wazazi, mama Maria na Yosefu, wakawapasha walioambiwa.

3

Wakijiunga nao majeshi ya mbinguni, wote waliimba
sifa kwa Mungu juu mbinguni, na amani kwa watu anaowapenda.